

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

687

VITENDO VYA KUJIFUNZA HAIBA NA MICHEZO

Mwaka: 2020

Muda: Saa 3

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **manne (4)** kutoka sehemu B.
3. Sehemu A in jumla ya alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako ch **akujibia**.



## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Onesha hatua ambazo mwalimu wa Elimu ya Awali anatakiwa kuzifuata anapofundisha mchezo wa “nyama nyama nyama.”
2. Elezea kwa kifupi zana nne zinazoweza kutumika kufundisha watoto dhana ya nidhamu katika michezo.
3. Bainisha viashiria vinne vya nidhamu katika mchezo wanaocheza watoto.
4. Kwa kutumia hoja nne, eleza kwa kifupi kwa nini ni muhimu kuandaa azimio la kazi kabla ya muhula kuanza.
5. Toa hoja nne zinazoonesha namna ambavyo andalio la somo humsaidia mwalimu katika ufundishaji wake.
6. Elezea kwa kifupi umuhimu wa watoto wa Elimu ya Awali kujifunza Vitendo vya Haiba na Michezo. Toa hoja nne.
7. Kwa kutumia mifano, bainisha umuhimu wa kuhimiza na kuendeleza tabia njema kwa watoto. Toa hoja nne.
8. Kwa kutumia mfano, elezea kwa kifupi mbinu nne anazoweza kutumia mwalimu wa Elimu ya Awali kufundisha matendo ya tabia njema.
9. (a) Eleza kwa kifupi dhana ya zana za kufundishia kama inavyotumika katika somo la Vitendo vya Kujifunza Haiba na Michezo.  
(b) Fafanua kwa ufupi makundi matatu ya zana za kufundishia.
10. Chambua kwa kifupi changamoto kuu nne anazoweza kuzipata mwalimu wa Elimu ya Awali asipoandaa azimio la kazi.

## SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **manne (4)** kutoka sehemu hii.

11. “Maendeleo mazuri ya kitaaluma kwa mtoto hutegemea sana tabia njema ya mtoto.” Thibitisha usemi huu kwa hoja tano.

12. Kwa kutoa mifano, changanua mambo matano muhimu anayotakiwa kuzingatia mwalimu wakati wa kuchagua mbinu za kufundishia na kujifunzia.
13. Fafanua mbinu tano zinazoweza kutumika kurekebisha tabia za watoto wenye utovu wa nidhamu kila mara katika michezo,
14. "Matumizi ya viboko katika kudumisha nidhamu kwa watoto wa Elimu ya Awali yana hasara zaidi kuliko faida." Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja tano.
15. Maandalizi katika ufundishaji hasa wa watoto wadogo ni muhimu katika kumwezesha mwalimu kufundisha kwa ufanisi. Taja na eleza vifaa vitano ambavyo vitamsaidia mwalimu katika kuandaa andalio la somo.
16. Kwa kutumia hoja tano, eleza jinsi mwalimu anavyoweza kuendeleza matendo ya tabia njema kwa mtoto.